



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI

TANGAZO LA ZABUNI 02 APRILI 2022.  
02.04.2022

Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imepokea fedha kwa ajili ya Ujenzi wa **SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA MKOA** Inayojengwa Kata ya Solya hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni inawatangazia mafundi wote wenye uwezo wa kufanya kazi za **UFUNDI KUENZIA MSINGI HADI UMALIZIAJI (FINISHING) MASHARTI NA VIGEZO.**

1. Awe Fundi mwenye uwezo wa kufanya kazi za ujenzi wa majengo.
2. Awe na aoneshe uzoefu katika kazi za ujenzi wa majengo ya Serikali.
3. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri vipimo, michoro na ramani za majengo.
4. Awe tayari kuwajibika kwa gharama zake kwa uharibifu wa kazi ukitokea nje ya maelekezo ya Muhandisi ujenzi.
5. Aoneshe muda atakaotumia kukamilisha kazi.
6. Kabrasha la maombi linapatikana Halmashauri ya wilaya ya Manyoni Ofisi ya Manunuzi na Ugavi (PMU) kila muombaji anatakiwa kuchukua kabrasha hilo .
7. Maombi haya ni ya -:
  - Ujenzi wa Vyumba Viwili vya Madarasa – Majengo 2
  - Ujenzi wa Vyumba Viwili vya Madarasa na Ofisi – Majengo 3
  - Ujenzi wa Vyumba Viwili vya Madarasa na Vyoo – Jengo 1
  - Ujenzi wa Maabara ya Fizikia na Chumba cha Jiografia – Jengo 1

- Ujenzi wa Maabara ya Kemia na Biologia – Jengo 1
- Ujenzi wa Jengo la Matundu 16 ya Vyoo – Jengo 1
- Ujenzi wa Nyumba ya Mwalimu Vyumba 3 – Jengo 1
- Ujenzi wa Nyumba ya Mwalimu 2 IN 1 – Jengo 1
- Ujenzi wa chumba cha Jenereta – Jengo 1
- Ujenzi wa Bweni la Wanafunzi 120 – Majengo 5

Kila kazi itaombwa peke yake.

8. Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni siku ya **Ijumaa Tarehe 08 Aprili 2022 Saa 10:30 asubuhi (SAA NNE NA NUSU ASUBUHI)**.
9. Maombi yafungwe ndani ya bahasha kwa lakiri na kuwasilishwa ofisi ya Manunuzi na Ugavi Kwa anwani ifuatayo Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni S.L.P. 60, Manyoni .
10. Kila fundi anaruhusiwa kuomba jengo Moja Tu

NB

- HAKUNA MALIPO KWA MAFUNDI YATAKAYOLIPWA KAMA MALIPO YA AWALI (ADVANCE) KWANI MALIPO YATAFANYWA BAADA YA TATHMINI YA KAZI ILIYOFANYWA.
- AWE MWAMINIFU KATIKA UTENDAJI KAZI, MALI ZILIZOPO NA KUJALI KWA KUFANYA KAZI KWA WAKATI BILA SHURUTI.

  
Melkizedeck O. Humbe

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI.**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
MANYONI**